
# MAANDALIZI



# HUONGEZA THAMANI

Pastor James Kalekwa

# Maandalizi Huongeza Thamani.

James Kalekwa

**Orodha ya Yaliyomo**

Tabaruku ........................................................................ 4

Salamu na Utangulizi ..................................................... 5

SURA YA KWANZA: DHANA YA MAANDALIZI .. 7

Kanuni 5 kuhusiana na Maandalizi .............................. 8

AINA 2 KUBWA ZA MAANDALIZI ...................... 12

SURA YA PILI: MIFANO KUHUSU MAANDALIZI YA UJUMLA NA YA SIKU KWA SIKI ..................... 13

SURA YA TATU: MATOKEO YA MAANDALIZI NA KUONGEZA THAMANI ............................................. 19

Kuhusu Mwandishi: ...................................................... 22

Kuhusu New Vine Church: ............................................ 22

Mawasiliano na Mwandishi: .......................................... 23

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

# Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma

yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# SURA YA KWANZA: DHANA YA MAANDALIZI

Muda unaoutoa kwenye maandalizi unaeleza ni kwa kiasi gani unaamini uendako. Kina cha maandalizi kianaamua kina cha matokeo. Ukitegea kwenye maandalizi, utaumbuka kwenye uwanja wa Maisha.

Ukweli ni huu maandalizi hayavutii sana ndiyo maana hayapendwi na watu wengi, lakini wewe hautakuwa kwenye orodha ya watakaokataa maandalizi kupitia kitabu hiki.

Maandalizi na kuongeza thamani ni namna moja wapo ya kuwekeza katika Kristo, na kama utajiona unawekeza ndani ya Kristo ni kupitia maandalizi yako.

1 kor 9: 23-27 *“Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine. Je! Hamjui, ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate. Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi*

*wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa."*

Kuna namna ya kupiga mbio ili upate. Na hiyo namna ni maandalizi. Kile unachokifanya kabla ya kupiga mbio ndiyo huamua nini ufanye wakati wa kupiga mbio.

## Kanuni 5 kuhusiana na Maandalizi

1. **Muda mrefu hutumika kwenye maandalizi kuliko kwenye mchezo halisi mchezo wenyewe.**

Wanaocheza mpira wa miguu kwenye mechi ya dakika 90, hawakujiandaa kwa dakika 90, bali walijiandaa kwa zaidi ya dakika 90. Kijana wekeza ujana wako kwa Kristo na uruhusu ayapike maisha yako toka ndani kwenda nje kama sehemu ya maandalizi. Vijana wengi sana wanataka kuonekana jukwaani bila maandalizi, wengi wanataka kuonekana ni wahubiri bila muda wa kujiandaa, wengine

wanataka kuonekana ni “super stars” bila kuonekna kwenye maandalizi.

*Wanaoshinda kwenye mchezo wa Maisha (Uchumi, ndoa, utumishi n.k) ni watu waliowekeza muda mrefu kujiandaa kwenye eneo husika*

Wengi maisha yanawashinda kwasababu hawana maandalizi.

2. **Maandalizi hayavutii watazamaji kama mchezo halisi**

Hakuna mtu anagombea kununua tiketi kwenda kuangalia maandalizi, hakuna mtu atakushangilia kwenye kipindi cha maandalizi, wakati unajiandaa usitarajie watu watakushangilia.

Kuna nyakati ambazo hakuna mtu atakujua, hakuna mtu atakuimba kinywani mwake, wewe binafsi unaweza kujiona upo vizuri lakini hakuna mtu anakujua. Maandalizi ni kipindi ambacho dunia haikujui, ni kipindi ambacho hakivuti watazamaji, usilazimishe kuwekwa kwenye mabango, usitafute kuonekana wakati wa maandalizi. Vijana wengi wametegwa hapo, wanataka

kuonekana kabla ya maandalizi au ya kipindi cha maandalizi.

Daudi alitumia muda wake wa maandalizi vyema, aliutumia machungani kuua simba na dubu kiasi kwamba alipowekwa mbele ya Goliath hakuaibishwa, na namna aliyomuua Goliath ilikuwa rahisi zaidi ya namna alivyowaua simba na dubu walipotaka kuchukua kondoo. Kipindi anaua simba na dubu hakuna aliyemwona wala kumsifia.

Maandalizi sio kipindi cha kuonekana. Ukiona unashangiliwa kwenye maandalizi ujue upo karibu na kuangamia/kupotezwa. Wakati wa maandalizi jizuie, *"Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote;"*

3. **Maandalizi huambatana na maumivu mengi kuliko mchezo halisi/wenyewe.**

*"Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha;"*

Kwenye maandalizi usilishe shauku yako. Kama unaenda mbali kwenye haya maisha kaa kwenye maandalizi kwa

sababu wanaoenda mbali hawalishi hamu zao, hamu ya usingizi, hamu ya chakula, na vionjo vingine visivyo na mchango wowote kwenye hatima yako.

Lazima uumie kwenye maandalizi. Ukitaka kula vizuri wakati wa ujana unakula hatima yako. Ina faida gani kula ikiwa unakula hatima yako?.

Ukweli ni kwamba: Maandalizi huwa hayamtupi mtu. Kama tu jembe lisivyomtupa mkulima.

4. **Unachokiona kwenye uwanja wa michezo ni matokeo ya kurudiarudia**

Unachokiona kinaonyeshwa jukwaani ni matokeo ya kurudia tena na tena sirini. Ili uweze kuitwa mbobevu kwenye jambo fulani ni lazima uwe umefannya kwa kurudia-rudia mpaka uweze kufanya bila kujifikiria mara mbili. Sasa, ukweli wa mambo ni kwamba kurudia rudia jambo moja kunachosha. Mwanadamu hupenda kujaribu mambo mapya. Usiuingie huo mtego!

Ukikwepa kurudia jambo mara nyingi ni ujumbe kwamba unakwepa kuwa mbobevu katika jambo hilo.

5. **Kiwango cha maandalizi kinaamua kiwango cha matokeo.**

Kwa kadiri unavyojiandaa inaonyesha utakuwa na matokeo kiasi gani, na kwa kadiri ambavyo haujiandai inaonyesha jinsi gani utakuwa na matokeo dhaifu.

Umri wa ujana ni umri wa maandalizi, ni umri wa kuwekeza.

Maandalizi yoyote ya kimaisha unayoyafanya sasa hivi, yanaelezea ni wapi unaenda siku za usoni. Wewe ni nabii wa uzee wako. Ukitaka kujua utakuwa mzee wa namna gani, angalia maandalizi yako.

## AINA 2 KUBWA ZA MAANDALIZI

1. Maandalizi ya Ujumla

Haya unajiandaa mara moja na inakuwa imeisha (once and for all)

2. Maandalizi ya siku kwa siku (mtindo/mfumo wa Maisha)

Haya unajiandaa siku kwa siku na unayafanya yanakuwa mtindo wako wa maisha.

# SURA YA PILI: MIFANO KUHUSU MAANDALIZI YA UJUMLA NA YA SIKU KWA SIKI

1. BWANA YESU

Mt 4:1-11 “Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako. Kisha Ibilisi akamchukua mpaka

mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake. Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia."

Tunamwona Bwana Yesu anawekeza siku arobaini za kufunga na kuomba kutengeneza kesho ya huduma yake ya hapa duniani kama maandalizi ya ujumla.

Wekeza muda kujiombea, wekeza muda kwajili ya kesho yako. Yale unayoyatamani yaliyo mbele wekeza muda kuyaombea, huyo mke muombee, huyo mume muombee. Ni ndoa, Uchumi, huduma, kazi.

Lk 4:14 *"Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando"*

Maandalizi ya jumla yanakupa nguvu ya kuenea wewe na habari zako, nguvu ya matokeo hazizaliwi kwa swaga, mtu ambaye ataenea na kuwa na matokeo ni mtu aliyefanya maandalizi ya kina.

Lk 22:39 *"Akatoka akaenda mpaka mlima wa Mizeituni kama ilivyokuwa desturi yake; wanafunzi wake nao wakafuatana naye."*

Yesu ilikuwa ni desturi yake kuomba siku kwa siku, ilikuwa ni desturi yake kuomba mara kwa mara. Unataka kuwa na matokeo fanya maandalizi, zika muda wako kujiandaa, unataka kuwa na matokeo ya kawaida usifanye maandalizi. Haya ni maandalizi ya siku kwa siku ya Bwana Yesu.

2. Mtumishi John G Lake (A man of healing faith), kitabu The Gods' Generals

Anaelezea habari ya maisha yake kuwa amekuwa katika mazingira ambayo ni magonjwa na vifo vimewazunguka watu, alifiwa na watoto wake na mke wake aliugua. Katika kipindi hicho ndipo akaamua kutafuta suluhisho la magonjwa kwa njia ya kumtafuta Bwana na alipata

suluhisho kiasi kwamba anafahamika kama mtu mwenye Imani ya uponyaji.

Historia yake iliuvuruga moyo wake kiasi kwamba alichukia magonjwa na hakukubaliana na njia za kisayansi za wakati za tiba. Hii ni kwa sababu aliwasikia watoahuduma wa afya kwenye vikao vyao wakionyesha ni kwa namna gani hata wao hawana uhakika na njia wanazotumia kutoa tiba bali wanafanya makisio tu.

Una historia gani, acha kukaa na kulialia, hesabu hiyo historia kuwa uwanja wa maandalizi na chukua hatua kutenda kutokea kwenye maandalizi hayo.

3. Usain Bolt

Nimeona nikuletee mfano wa mwanadamu ambaye unaweza kuwa unamfahamu. Lengo langu ni kukuonyesha hili ni jambo linalowezekana kutendeka. Anakubalika kuwa mwanariadha mashuhuri wa mbio fupi duniani, anashikilia rekodi ya kuwa mwanadamu mwenye kasi zaidi kuliko wanadamu wote duniani.

Anaeleze kuwa amejiandaa mafichoni huko nchi ya Jamaika kwa miaka 20, lakini kwa maandalizi yote hayo ya miaka 20 alikuja kucheza kwenye mashindano ya olimpiki na kutumia jumla ya muda wa dakika 2 tu (Hii ni sawa na sekunde 115). Ni ajabu sana kujiandaa miaka 20 kuja kucheza dakika 2.

Watu wengi tunashindwa kwa kuwa tunajiandaa dakika 2 ili tuje tushindane miaka 20 kitu ambacho hakina uwiano kabisa.

Usain Bolt kwa jumla ya dakika hizo 2 tu na ameshinda medali jumla ya medali 9 za dhahabu kwa mashindano ya olimpiki aliyoshiriki. Amepata jumla ya $119Milioni sawa na Tilioni 273Tzs. Siri ya matokeo yake ni maandalizi. Sasa hivi kila anachokigusa kinageuka kuwa dhahabu.

Usain Bolt hufanya mazoezi kwa siku 6 ndani ya wiki moja, kwa miezi 11 ndani ya mwaka. Hufanya mazoezi kwenye kwa jumla ya dakika 90 kila siku. Hufanya mazoezi ya kasi, nguvu na uvumilivu. Sehemu kubwa ya

mazoezi yake ni kujenga misuli ya muhimu na kuongeza nguvu.

Wekeza muda wa kutosha kwenye maandalizi yako.

Watu wote tunafanana kwa mwonekano. Kinachoamua tofauti kati ya mtu na mtu ni thamani, kama ni miguu wote tunayo, mikono wote tunayo na viungo vinigine wote tunavyo, ongeza thamani ili kujipambanua mwenyewe.

Tofauti yetu ni thamani yetu. Thamani yetu ni matokeo ya kiwango cha maandalizi tulichoweka.

Ujana ni wakati wa kuongeza thamani, usipokuwa na thamani watu wataanza kukukwepa. Kwenye chochote unachokifanya ongeza thamani ya maisha yako.

Swali gumu kwa mabinti: Tofauti na kuonyesha midomo na kujibinua na umbo, una kitu gani kingine cha kuonyesha kwenye ndoa? Hapa ndiyo utaona wadada wengi wanaweza kuvutia wanaume kimwili ila hawawezi kuolewa kwakuwa hawana thamani ya mke, hawafai kuwa mke.

Tafuta na ongeza thamani yako.

# SURA YA TATU: MATOKEO YA MAANDALIZI NA KUONGEZA THAMANI

1. Kufahamika kama mjuzi au mbobevu kwenye jambo Fulani

2Nyak 2:11-14 "*Ndipo Hiramu mfalme wa Tiro akajibu kwa waraka, aliompelekea Sulemani, Ni kwa sababu BWANA awapenda watu wake, amekufanya uwe mfalme juu yao. Hiramu akasema tena, Na ahimidiwe BWANA, Mungu wa Israeli, aliyezifanya mbingu na nchi, ambaye amempa mfalme Daudi mwana wa hekima, mwenye busara na akili, ili amjengee BWANA nyumba, na nyumba kwa ufalme wake. Na sasa nimemtuma mtu mstadi, mwenye akili, yaani, Hiramu baba yangu, mwana wa mwanamke wa binti za Dani, na babaye alikuwa mtu wa Tiro, ajuaye sana kazi ya dhahabu, na ya fedha, ya shaba, ya chuma, ya mawe, na ya mti, ya urujuani, ya samawi, na ya kitani safi, na ya nyekundu;* ***tena mstadi wa kuchora machoro yo yote, na wa kufikiri fikira yo yote;***

***apate kuagiziwa kazi pamoja na watu wako wastadi, tena na wastadi wa bwana wangu Daudi baba yako.***"

Hakikisha unajulikana kuwa mtaalamu wa eneo fulani. Tunamwona Hiramu anafahamika kama mtaalamu wa kufikiri fikira yoyote na kuchora machoro yoyote. Maandalizi na kuongeza thamani kunakupa kufahamika kama mbobevu kwenye eneo Fulani.

2. Maandalizi na kuongeza thamani kunakusababisha kutenda kazi pamoja na wafalme.

Tunamwona Hiramu anafanya kazi na mfalme tajiri kuliko matajiri waliowahi kutokea na watakaowahi kuwepo.

Kila mtu aliyewekeza kwenye maandalizi kiasi cha thamani yake kuongezeka, amejihakikishia kiti kwenye kikao cha wafalme na watu wakuu.

3. Unakuwa na uhakika wa matokeo

Waamuzi 20:16 BHN *"Kati ya watu hao waliochaguliwa kulikuwa na watu 700* ***waliotumia mkono wa kushoto****;* ***kila mmoja aliweza kurusha jiwe kwa kombeo na kulenga unywele bila kukosea****."*

Maandalizi na kujiongezea thamani yanakufanya uwe na uhakika wa kuzalisha matokeo fulani; Uwe na acuuracy katika utendaji wako… uwe unaweza kulenga na kupata! Watu wa namna hii wakianzisha jambo fulani halifi, hata shetani awe analala mlangoni mwa biashara yao haiwezi kufa.

Jiulize: ni kitu gani unaweza kulenga bila kukosea? Ni eneo gani unaweza kufanya maamuzi bila kukose? Ni maamuzi mangapi umewahi kufanya bila kukosea?

Watu wengi hawana uhakika na maamuzi yao wenyewe.

Ukifanya maandalizi na kujiongezea thamani matokeo yanakuwa ya uhakika.

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764